







*IDARA YA UPATIKANAJI WA AFYA YA VERMONT*

# Mipango ya Duka la Dawa
# Kitabu cha mwongozo

GreenMountainCare
A HEALTHIER STATE OF LIVING

# Attention! If you need help in your language, please call 1-800-250-8427

انتباه! إذا كنت بحاجة إلى مساعدة بلغتك ، فيرجى الاتصال
على 1-800-250-8427

သတိပြုရန်! မိတ်ဆွေသည် သင့်ဘာသာစကားဖြင့် အကူအညီ လိုပါက၊
ကျေးဇူးပြုပြီး 1-800-250-8427 ကိုခေါ်ပါ။

Pažnja! Ako vam je potrebna pomoć na vašem jeziku, pozovite **1-800-250-8427**

توجه! اگر شما نیاز به کمک در زبان خود، لطفا با شماره تلفن 1-800-250-8427

Attention! Si vous avez besoin d’assistance dans votre langue, appelez le **1-800-250-8427**

Nurabe maso! Niba ukeneye ubufasha mu rurimi rwawe, wahamagara kuri **1-800-250-8427**

ध्यान! यदि तपाईंलाई आफ्नो भाषामा मद्दत चाहिन्छ भने, कृपया **1-800-250-8427** मा कल गर्नुहोस्

پاملرنه! که تاسو په خپله ژبه کې مرستې ته اړتیا لرئ،
مهرباني وکړئ **1-800-250-8427** ته زنګ ووهئ

Ogow! Haddii aad u baahan tahay in lagugu caawiyo luqaddada, fadlan wac **1-800-250-8427**

¡Atención! Si necesita ayuda en su idioma, por favor llame al **1-800-250-8427**

Muhimu! Kama unahitaji msaada kwa lugha yako, tafadhali piga simu **1-800-250-8427**

Uvaha! Yakshcho vam potribna dopomoha vashoyu movoyu, telefonuyte za nomerom **1-800-250-8427**

# Yaliyomo


Karibu kwenye Mpango wako wa Duka la Dawa wa Vermont ........ 5
Mpango wa Afya wa Wakazi wa Vermont ........ 5
Mipango ya VPharm: VPharm 1, VPharm 2 na VPharm 3 ........ 5
Kuelewa PDP yako ya Medicare ........ 5
VPharm 1: Malipo na Bima ........ 6
VPharm 2: Malipo na Bima ........ 6
VPharm 3: Malipo na Bima ........ 6
Mfumo wako wa PDP ya Medicare ........ 7
Dawa Zisizojumuishwa na Medicare, Dawa za kununua dukani (OTC) ........ 7
Malipo ya ushirika (au malipo ya kushirikiana) ........ 7
Kitambulisho chako ........ 7
Watoa huduma Wanaoshiriki ........ 8
Mipango ya Duka la Dawa kwa Wakazi wa Vermont na Medicare ........ 8
Mipango ya Akiba ya Medicare ........ 8
Mnufaika Anayestahiki kwenye Medicare (QMB) ........ 8
Wanufaika wa Medicare wenye Mapato Madogo Yaliyobainishwa (SLMB) ........ 8
Watu Wanaostahiki (QI-1) ........ 8
Kulipa Malipo Yako ........ 8
Malipo ya Moja kwa Moja ........ 8
Haki na Wajibu Wako ........ 9
Mipango Mingine kwa Wakazi wa Vermont ........ 10
Wosia na Maagizo ya Mapema ........ 10
Uchangiaji wa Viungo ........ 11
Kutoa Taarifa kwa Mtoa Huduma wako ........ 11
Notisi ya Shughuli za Faragha ........ 11
Mpango wa Hakikisho la Ubora ........ 11
Matatizo na Malalamiko ........ 12
Unapokuwa Hukubaliani na Kitendo ........ 12
Kukata rufaa dhidi ya Kukataliwa na PDP yako ya Medicare ........ 12
Kukata rufaa dhidi ya Kukataliwa na VPharm ........ 13
Usikilizaji wa Haki kwa Kukataliwa kwa Rufaa ya DVHA ........ 14
Kuendelea na Mafao ........ 15
Malalamiko ........ 15
Sababu za Msingi na Ombi la Ugumu ........ 16
Je, Unahitaji Msaada? ........ 16
Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Vermont Health Connect, Green Mountain Care ........ 16
Kuripoti Mabadiliko ........ 16
Ofisi ya Utetezi wa Huduma za Afya (HCA) ........ 17
Taarifa za Ziada ........ 17
Mipango Mingine Isiyo ya Dawa ........ 17
Huduma za Mchana kwa Watu Wazima ........ 17

Mpango wa Huduma za Wahudumu ....17
Huduma Jumuishi za Watoto (CIS) ....17
Huduma Jumuishi za Watoto - Afua ya Mapema (CIS-EI) ....18
Huduma za Matunzo Binafsi ya Watoto (CPCS) ....18
Kliniki za Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Afya (CSHN) ....18
Machaguo ya Uangalizi ....18
Huduma za Ulemavu wa Ukuaji ....19
Mpango wa Msaada wa Kifedha ....19
Ufadhili Rahisi wa Familia ....19
Huduma za Uuguzi za Teknolojia ya Hali ya Juu ....19
Mpango wa Huduma ya Nyumbani ya Taknolojia ya Hali ya Juu kwa Watoto ....19
Huduma za Wahudumu wa Nyumbani ....19
Kliniki Maalum ....19
Huduma Maalum ....20
Mpango wa Vermont wa Kugundua na Afua ya Mapema wa Kusikia ....20
Afya ya Akili ....20
Huduma kwa Wagonjwa wa Nje Ambao ni Watu Wazima ....20
Huduma za Watoto, Vijana na Familia ....21
Ukarabati wa Jamii na Matibabu ....21
Huduma za Dharura ....21
Mpango wa Majeraha ya Kiwewe cha Ubongo ....21
Mpango wa Wanawake, Watoto wachanga na Watoto (WIC) ....21
Rasilimali za Ziada katika Jamii Yako ....22
Udanganyifu, Uharibifu, na Dhuluma ....22

Oktoba 2024

# Karibu kwenye Mpango wako wa Duka la Dawa wa Vermont

Mipango ya dawa Vermont inasimamiwa na Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont. Imeorodheshwa hapa. Kila mtu una kanuni na mafao yake.

**Kitabu hiki cha mwongozo hakina taarifa juu ya mafao ya famasia za Medicaid.** Je, una Medicaid na unahitaji taarifa kuhusu mafao yako ya dawa? Je, hujui upo katika mpango gani? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** Piga simu Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa 2 asubuhi (8:00 a.m) hadi saa 10:30 jioni (4:30 p.m.) (kunafungwa siku za sikukuu).

## Mpango wa Afya wa Wakazi wa Vermont

Huu ni mpango wa bure kwa wakazi wa Vermont bila bima ya dawa uliyoandikiwa na daktari. Inawawezesha kununua dawa zinazolipiwa na bima kwa gharama nafuu. Je, una Healthy Vermonters? Duka lako la dawa linaweza kuwasilisha madai kwenye Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont. Idara haitafanya malipo. Lakini utalipa kiwango cha chini cha Medicaid, sio bei ya rejareja ya duka la dawa.

## Msaada wa Mapato ya Chini (LIS) au "Msaada wa Ziada"

Mpango huu husaidia kulipa gharama za dawa kwa watu kwenye mpango wa dawa wa Medicare. Inalipa malipo ya kila mwezi, makato ya kila mwaka, na malipo ya ushirika ya dawa. Gharama zingine hazilipwi na mpango wa dawa au Msaada wa Ziada. Green Mountain Care itasaidia kulipa baadhi ya gharama hizo. Je, wewe upo katika Mpango wa Akiba wa Medicare? Basi tutakusajili kwa Msaada wa Ziada. **Watu wengine lazima waombe Msaada wa Ziada kila mwaka.**

**Unataka kujiandikisha au kujifunza zaidi?** Piga simu kwenye ofisi yako ya Mpango wa Msaada wa Bima ya Afya ya Jimbo kwa **1-800-642-5119**. **AU** piga simu kwenye ofisi yako ya Usalama wa Jamii au nenda kwenye tovuti hii.

## Kuelewa Mpango Wako wa Dawa Medicare Uliyoandikiwa na Daktari

Kwa kawaida huu ni Mpango wa Dawa wa Sehemu D ya Medicare. Unaweza pia kuwa sehemu ya mpango wa Medicare Sehemu C au "Medicare Advantage". Hizi zote mbili huitwa Mpango wa Dawa wa Medicare Ulioandikiwa na Daktari. Vituo vya Huduma za Medicare na Medicaid vinaendesha mipango hii. Ikiwa unahitaji msaada kupata Mpango wa Dawa ya Maagizo wa Medicare:

1) Piga simu **1-800-633-4227** - TTY 1-877-486-2048
2) **AU** nenda kwenye Tovuti ya Medicare.
3) **AU** Piga simu kwenye Mpango wa Msaada wa Bima ya Afya ya Jimbo **1-800-642-5119.** Wako kwenye Shirika la Eneo Husika la Msaada wa Wazee.

## Mipango ya VPharm: VPharm 1, VPharm 2 na VPharm 3

Mipango ya VPharm husaidia watu ambao hawawezi kupata Medicaid lakini wana Medicare. Hulipia Mpango wao wa Dawa wa Medicare na gharama zinazohusiana. Utakuwa na malipo ya ushirikiano ya $ 1 au $ 2, kulingana na dawa. VPharm hulipia gharama iliyobaki.

**VPharm pia inaweza kusaidia kulipa malipo ya kila mwezi kwenye mpango wako wa dawa wa Medicare.**

VPharm ina viwango 3: VPharm 1, VPharm 2, na VPharm 3. Kila mpango una sheria na faida zake. Mpango wako wa dawa wa Medicare hulipia sehemu yake kwa dawa zako zote. Unalipa malipo yako ya ushirika. Kisha VPharm inalipia sehemu yake. Wanachama lazima wawe na mpango wa dawa wa Medicare ili kuendelea na VPharm. Mpango wako wa dawa lazima ufanye kazi katika jimbo la Vermont. Lazima utumie mtoa huduma wa Vermont Medicaid.

## Malipo ya Kila mwezi ya Bima:

- **$ 15** kwa VPharm 1
- **$ 20** kwa VPharm 2
- **$ 50** kwa VPharm 3

## VPharm1, VPharm 2 na VPharm 3 yote hulipia:

- **Vifaa vya Kisukari**
- **Sehemu ya mpango wako wa dawa malipo ya kila mwezi hadi gharama iliyowekwa**. Serikali kuu huamua gharama iliyowekwa kila mwaka Januari 1. Msaada wa Mapato ya Chini (LIS) "Msaada wa Ziada" pia hulipia sehemu ya malipo ya kila mwezi. Je, wewe una mpango ulioimarishwa wa dawa wa Medicare? Basi VPharm haiwezi kulipa malipo kamili ya kila mwezi.
- **Sehemu ya malipo yako ya ushirikiano, makato na bima ya ushirikiano NA mapungufu ya bima kwa dawa za muda mfupi na za muda mrefu**. Msaada wa Mapato ya Chini "Msaada wa Ziada" pia hulipia sehemu ya gharama hizi.
- **Baadhi ya dawa ambazo hazijajumuishwa kwenye mpango wa dawa**. Hii ni baadhi ya dawa za kununuliwa dukani, vitamini na dawa za kikohozi/mafua.

## VPharm 1 pia inalipia:

- **Uchunguzi wa macho** mmoja wa kina na mmoja wa mpito kila baada ya miaka 2. Unapaswa kufanywa na mtaalamu wa macho au daktari wa macho.

**Unataka taarifa zaidi au kujisajili kwa ajili ya VPharm 1, VPharm 2 au VPharm 3?** Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Piga Simu Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa 2:00 asubuhi (8:00a.m.) hadi 10:30 jioni (4:30p.m.). Hatufanyi kazi siku za sikukuu.

## Mfumo wako wa Mpango wa Dawa

A **mfumo** ni orodha ya dawa. Ili kusaidia kupunguza gharama, mpango wako wa dawa unawaomba madaktari kuandika maagizo ya dawa kutoka kwenye orodha hii. Kwa baadhi ya dawa, mpango wako wa dawa lazima uidhinishe dawa kabla ya kuipata. Hii inaitwa **idhini ya awali**. Bila kufanya hivyo, hawatalipia gharama za dawa. Ikiwa mpango wako wa dawa hautaidhinisha dawa, unaweza kukata rufaa. Angalia sehemu "Wakati Hukubaliani na Hatua Hiyo."

## Medicare Hawatalipia Baadhi ya Dawa

Hizi zinaitwa **Dawa za Zisizojumuishwa na Medicare**. Inajumuisha dawa za kununua dukani, baadhi ya vitamini zinazoagizwa na daktari na dawa za kikohozi na mafua. Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont inalipia baadhi ya dawa hizi lakini zingine zinahitaji idhini ya awali. Daktari wako anaweza kuomba idhini ya awali. Wanapaswa kukajaza fomu ya idhini ya awali na kuituma. Wanaweza kupata fomu hiyo katika Tovuti ya Medicare.

VPharm inalipia **baadhi** ya dawa za kawaida za kununua dukani. Hii hapa niorodha kamili.

Mipango yetu **haijumuishi** dawa za majaribio kwa sababu hakuna uthibitisho kwamba zinafanya kazi. Pia, hatujumuishi dawa ambazo hazijaidhinishwa na Mamlaka ya Dawa ya Serikali Kuu.

## Malipo ya ushirika au malipo ya kushirikiana

Ukiwa na VPharm, malipo yako ya ushirikiano kwa kila dawa yatakuwa $1 au $2.

- Ikiwa jimbo linalipa $29.99 au chini yake kwa dawa hiyo, malipo yako ya ushirikiano yatakuwa $1.
- Ikiwa jimbo litalipa $30 au zaidi kwa dawa hiyo, malipo yako ya ushirikiano yatakuwa $2.

Itakuwaje ikiwa unaambiwa ulipe zaidi ya $ 2? Muulize mfamasia wako kama aliwaandikia bili Green Mountain Care. Au Piga Simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427** kwa msaada.

## Kitambulisho Chako

Kitambulisho chako cha Green Mountain Care itatumwa nyumbani kwako. Tafadhali onyesha unapokuwa unapoenda kwenye duka la dawa. Je, hukupata kadi yako mpya ya kitambulisho ndani ya mwezi mmoja baada ya kupata kitabu hiki cha mwongozo? **AU** umepoteza kadi yako? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427** na uombe kadi mpya.

Je, una bima ya dawa za Medicare? Kisha onyesha mtoa huduma wako kadi zako zote za bima.

### Madaktari na Watoa Huduma

Madaktari ambao wanakuandika maagizo ya dawa na duka lako la dawa **lazima** wawe sehemu ya mipango yetu. Madaktari na maduka mengi ya dawa katika jimbo la Vermont tayari yapo. Je, una maswali kuhusu madaktari na maduka ya dawa? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427. AU** Nenda kwenye tovuti na ubonyeze "Utafutaji wa Mtoa huduma."

## Mipango ya Akiba ya Medicare

Hii ni mipango ambayo huwasaidia watu kulipa kwa ajili ya Medicare Sehemu A na Sehemu B. Baadhi ya wanachama wa VPharm wenye mapato ya chini wanaweza kupata msaada wa kulipia gharama zote. Je, unataka Medicare na Medicaid zikusaidie kulipa? Basi madaktari/watoa huduma wako lazima wawe sehemu ya mipango ya Medicare na Medicaid. Mipango ni:

- **Mnufaika Anayestahiki kupata Medicare (QMB)** - Hulipia malipo ya kila mwezi ya Medicare Sehemu A na B, makato, bima ya ushirikiano, na malipo ya ushirikiano
- **Wanufaika wa Medicare wa Mapato ya Chini Yaliyobainishwa (SLMB)** - Hulipia malipo ya kila mwezi ya Medicare Sehemu B pekee
- **Watu Wanaostahiki (QI-1)** - Hulipia malipo ya kila mwezi ya Medicare Sehemu B pekee

**Haulipi malipo ya kila mwezi kwa Mipango ya Akiba ya Medicare.** Barua kuhusu bima yako ya VPharm ilisema ikiwa unaweza kupata msaada huu. Vipi ikiwa huna Mpango wa Akiba wa Medicare lakini unafikiri unauhitaji? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

## Lipa Malipo Yako ya Kila Mwezi ya VPharm

Lipa mara tu unapopokea bili ya kwanza. Ikiwa unafanya hivyo, bima inaweza kuanza kutumika mwanzoni mwa mwezi ujao. Lazima uendelee kulipa kwa wakati. Hivyo, hutapoteza au kuwa na pengo katika bima yako. Wanachama wa Mpango wa Healthy Vermonters **Hawana** malipo ya kila mwezi. Lakini mipango mingine yote ya maduka ya dawa inayo.

Itakuwaje ikiwa unapoteza bili yako? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** Wanaweza kukuambia ni kiasi gani unadaiwa na jinsi ya kulipa.

### Unaweza kupanga Malipo ya Moja kwa Moja

Hivyo, huhitaji kuwa na wasiwasi juu ya kulipa bili yako kila mwezi. Malipo yako yatachukuliwa kutoka kwenye akaunti yako ya hundi au akiba kila mwezi.

Una maswali kuhusu malipo yako ya bima ya kila mwezi? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** Wanaweza pia kukuambia juu ya kuweka malipo ya moja kwa moja.

# Haki na Wajibu Wako

**Una haki ya:**

- Kutendewa kwa adabu.
- Kutunzwa kwa uangalifu.
- Kuchagua na kubadilisha daktari/watoa huduma wako.
- Kupata ukweli kuhusu huduma za mpango wako na daktari/watoa huduma.
- Kuambiwa kuhusu afya yako kwa maneno ambayo unaweza kuyaelewa.
- Kuamua kuhusu huduma yako ya afya, kujibiwa maswali yako, na kukataa matibabu.
- Kuuliza na kupata nakala ya taarifa zako za matibabu. Unaweza kuomba mabadiliko kama taarifa si sahihi.
- Pata maoni ya pili kutoka kwa daktari/watoa huduma mwingine aliyejiandikisha katika Vermont Medicaid.
- Zungumza kuhusu mpango wako au wasiwasi wa huduma za afya.
- Kutozuiliwa au kutotengwa kwa sababu ya uonevu, adhabu, au kwa sababu ni rahisi zaidi.
- Omba rufaa ikiwa umenyimwa huduma unazofikiri unahitaji. Angalia ukurasa wa 12 kwa taarifa zaidi.

## Tunza afya yako kwa:

- Kumwambia daktari wako kuhusu dalili zako za ugonjwa na historia ya afya.
- Kuuliza maswali unapohitaji kujua zaidi au unapokuwa huelewi kitu.
- Kufuatia mipango ya matibabu ambayo wewe na daktari wako mnakubali.
- Kutekeleza miadi yako au kupiga simu mapema ili kughairi kama huwezi kufika.
- Kufahamu kuhusu kanuni za mpango wako ili utumie huduma bora uwezavyo.
- Kuhakikisha unapata rufaa zinazohitajika kutoka kwa daktari wako kabla ya kuona madaktari wengine.
- Kulipa malipo ya bima na malipo ya ushirikiano kama inavyohitajika.

# Mipango Mingine kwa Wakazi wa Vermont

## Wosia na Maagizo ya Mapema

**Wosia** ni taarifa ya maandishi. Unasema:

- Je, ni nani anayeweza kukufanyia maamuzi ya kiafya unapokuwa huwezi
- Ni kiasi gani mtu anaweza kuamua
- Daktari/mtoa huduma wako wa msingi ni nani
- Ni huduma gani za afya na au matibabu unayotaka
- Jinsi unavyotaka masuala binafsi yashughulikiwe, kama vile mazishi yako
- Nani unayemtaka kuwa mlinzi wako, ikihitajika
- Nani **usiyemtaka** kufanya maamuzi kwa ajili yako
- Unataka uangalizi wa aina gani kama unakufa

Wosia ni bure. Pia huitwa mwongozo wa mapema au mamlaka ya kudumu ya uwakilishi kwa huduma ya afya. Zinaweza kuitwa hati ya uangalizi wa mwisho wa maisha. Sheria ya Vermont kuhusu wosia ni sheria ya Maagizo ya Mapema ya Vermont (Andiko la 18, Sura ya 231).

Unaweza kuwa mgonjwa sana kiasi cha kushindwa kufanya maamuzi ya afya. Ikiwa **hakuna** dharura, Madaktari hawawezi kukupa huduma papo hapo. Ni lazima kwanza wajue kama una wosia. Ikiwa unao, lazima watii maelekezo katika wosia. **AU** watii maelekezo ya mtu uliyemchagua kufanya maamuzi ya afya.

Je, daktari anaweza kukataa kufuata maelekezo katika maagizo yako ya mapema? Ndiyo, ikiwa wanaamini kuwa si sahihi. **LAKINI** lazima:

- Wakwambie wewe na mtu uliyemtaja kufanya maamuzi;
- Kusaidia kuhamisha huduma yako kwa daktari mwingine ambaye atatii maelekezo;
- Kuendelea kukupa huduma za afya hadi daktari mpya apatikane; na
- Kueleza katika taarifa yako ya matibabu:
    - tatizo
    - hatua zilizochukuliwa ili kuirekebisha na
    - jinsi tatizo lilivyotatuliwa.

Kila mhudumu wa afya lazima atii sheria ya wosia. Ni lazima wawe na kanuni zao ili kuhakikisha sheria na kanuni zinafuatwa.

Je, unafikiri kuna mtu hafuati sheria? Piga simu kwenye Idara ya Leseni na Ulinzi kwa **1-800-564-1612. AU** Nenda kwenye tovuti ya Idara ya Leseni na Ulinzi ili kuwasilisha malalamiko. **AU t**uma barua kwa:

Idara ya Leseni na Ulinzi
103 South Main Street, Ladd Hall
Waterbury, VT 05671

Je, unataka taarifa kuhusu sheria ya nchi na wosia? Piga simu kwenye Mtandao wa Maadili wa Vermont kwa **1-802-828-2909. AU** nenda kwenye tovuti yao kwenye **vtethicsnetwork.org**. Pia wana fomu za kuandaa wosia.

Andiko la 18 ni sheria ya Vermont kuhusu wosia. Unaweza kuiona mtandaoni. Unataka kujua zaidi? Zungumza na daktari wako au piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

## Uchangiaji wa Viungo

Unaweza kutaka kutoa ufadhili wa viungo vyako unapokufa. Mchangiaji mmoja anaweza kusaidia watu wengi. Ili kupata maelezo zaidi, piga simu kwa **1-888-275-4772** kwa taarifa bila malipo. Au tembelea tovuti kwa taarifa za bila malipo.

### Kutoa Taarifa kwa Daktari/Mtoa huduma wako

Tunataka kumsaidia daktari wako kuhakikisha kwamba unapata huduma ya afya unayohitaji. Tunaweza kuwapa orodha ya dawa unazozitumia. Hii husaidia kuhakikisha kwamba unapata dawa ambazo zinafanya kazi vizuri kwa pamoja kwako.

## Notisi ya Shughuli za Faragha

Umepokea barua inayosema kuwa umetimiza sheria za programu zetu. Pia ilikuwa na nakala ya **Notisi yetu ya Shughuli za Faragha.** Sheria ya serikali kuu, inayoitwa HIPAA, inasema lazima tukupe notisi. Notisi inakuambia haki zako za faragha. Inasema jinsi taarifa zako za afya zinavyoweza kutumiwa au kutolewa. Je, unahitaji nakala nyingine ya notisi? Piga Simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427** na uiombe. **AU** Unaweza kuiona mtandaoni.

## Mpango wa Hakikisho la Ubora

Huu ni mpango wa kuhakikisha kwamba unapata uangalizi bora wa afya na huduma bora. Baadhi ya mambo tunayoangalia ili kuhakikisha ni:

- Wagonjwa wanatumia dawa kiasi gani;
- Ni wanachama wangapi wanapata huduma ya mara kwa mara ili kuzuia magonjwa;
- Ni wanachama wangapi wanaotumia chumba cha dharura wakati **hakuna** dharura;
- Jinsi wahudumu wa afya ya mwili na akili wanavyofanya kazi pamoja;
- Jinsi wanachama na watoa huduma wanafurahishwa na programu zetu.

Tunawaomba madaktari kufuata miongozo yetu bora ya mazoezi kwa magonjwa fulani sugu. Hii inaweza kukufanya uwe na afya njema.

Je, kuna njia ambazo tunaweza kuboresha mipango yetu na kuifanya ikufanyie kazi vizuri zaidi? Piga simu Huduma kwa Wateja **1-800-250-8427**. Maoni yako yatakuwa sehemu ya ukaguzi wetu wa ubora.

### Matatizo na Malalamiko

Je, una matatizo ya kupata dawa zako za maagizo ya daktari? Au una malalamiko? Piga Simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Ikiwa tatizo lako halijatatuliwa, unaweza kukata rufaa. Pata maelezo zaidi kuhusu rufaa kwenye ukurasa wa 14.

## Ikiwa Hukubaliani na Uamuzi Kuhusu Dawa Zako

Mpango wako wa dawa utafanya maamuzi mengi zaidi. Piga simu kwa namba ya huduma kwa wateja iliyo nyuma ya kitambulisho. Watakueleza jinsi ya kukata rufaa ikiwa hukubaliani nayo. Hapa chini kuna maelezo ya jinsi ambavyo rufaa zinafanyika wakati una mpango wa dawa na VPharm.



### Kukata rufaa dhidi ya Kukataliwa na Mpango wako wa Dawa

**Je, uliomba idhini ya awali ya dawa? Je, mpango wako wa dawa ulikataa kulipa?** Unaweza kuomba VPharm kuilipia. **LAKINI** kwanza lazima ufuate sheria zote za rufaa za mpango wako wa dawa. Kuna hatua mbalimbali. Unapaswa kukata rufaa kila hatua ikiwa ni pamoja na hatua ya **Independent Review Entity**. Je, itakuaje ikiwa Independent Review Entity inasema mpango wa dawa hauhitaji kulipa? Basi daktari wako anayeandika maagizo ya dawa anaweza kuiomba VPharm kuilipia. Lazima watoe kwa VPharm nakala ya uamuzi wa Independent Review Entity.

**Je, mpango wako wa dawa haukulipia dawa yako kwa sababu "haijajumuishwa kwenye bima?"** Kama ni hivyo, basi wewe **huhitaji** kukata rufaa. Daktari wako atahitaji kuiomba VPharm kulipia. Lazima wawape VPharm nakala ya karatasi inayosema dawa hiyo haijajumuishwa kwenye bima.

**VPharm itatuma taarifa iliyoandikwa kwako na kwa daktari wako. Itasema walichoamua.** Je, itakuwaje ikiwa VPharm itaamua kukataa, kuzuia, kupunguza, au kusimamisha mafao? Hii inaitwa "uamuzi wa faida mbaya." Unaweza pia kuwaomba waangalie uamuzi huo tena. Hii inaitwa rufaa ya ndani. Endelea kusoma ili kujua zaidi.

## Je,Unadhani Uamuzi wa VPharm si Sahihi?

### Omba Rufaa ya Ndani

Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont pia inaitwa DVHA. Rufaa ya ndani inaomba DVHA kuangalia tena uamuzi wa VPharm uliofanywa. Mtu ambaye hakuhusika kufanya uamuzi wa kwanza ataangalia kesi yako. Watakuambia watakachoamua. Hii inaitwa rufaa ya ndani. Mara nyingi, lazima ufanye hivyo kabla ya kuomba Usikilizwaji wa shauri la Haki katika Jimbo.

Una **Siku 60** za kukata rufaa. Siku 60 huanza tarehe DVHA ilikutumia taarifa ya uamuzi. Mtoa huduma wako anaweza kuomba rufaa ikiwa utampa ruhusa ya maandishi. Unaweza kukata rufaa kwa maandishi au kwa simu.

**Kuna njia 3 za kuomba rufaa ya ndani:**

1. **Piga simu** Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** TDD/TTY: 1-888-834-7898
2. Mtandaoni: https://dvha.vermont.gov/members/appeals-and-fair-hearings/members AU Barua pepe.
3. **Tuma barua** kwa:

   Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont
   Timu ya Rufaa za Huduma ya Afya
   150 Pilgrim Park – 3rd Floor
   Waterbury, VT 05671-4030

**Je, tumepunguza au sitisha mafao yaduka la dawa ambazo tayari unapata?** Unaweza kuziendeleza wakati wa rufaa yako **ukiomba hivyo**. Lazima uombe hili kabla ya mabadiliko kuanza. Ni njia ipi bora ya kuendelea kupata huduma zako? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

**Nini kinatokea katika rufaa ya ndani?** DVHA itaandaa mkutano wa kuangalia tena uamuzi wake. Unapaswa kushiriki katika mkutano huu. Unaweza kujisemea mwenyewe au kuwa na mwakilishi. Mtoa huduma wako anaweza kuzungumza au kutoa taarifa kwa DVHA. **Je, Unahitaji Msaada?** Unaweza kupata ushauri wa kisheria wa bila malipo. Piga simu kwenye Ofisi ya Msaada wa Kisheria ya Utetezi wa Huduma za Afya kwa **1-800-917-7787.** Au nenda kwenye tovuti ya Msaada wa Kisheria kwenye intaneti.

**DVHA lazima iamue rufaa yako ndani ya siku 30.** Je, itakuwaje ukiomba muda zaidi? Je, itakuwaje ikiwa kusubiri kwa muda mrefu kunaweza kukusaidia? Mifano: Daktari wako anahitaji muda zaidi kutuma maelezo. Au huwezi kufika kwenye mkutano wakati huo. Basi inaweza kuchukua siku 14 zaidi . Muda mrefu zaidi ambao uamuzi utawahi kuchukua ni **siku 44**.

**Je, unahitaji DVHA kuamua rufaa yako haraka?** Tuambie ikiwa kusubiri kutaumiza sana afya au maisha yako. DVHA itaona kama unakidhi kanuni za rufaa ya haraka (inayoharakishwa). Ukifanya hivyo, utapata uamuzi **ndani ya saa 72**. Inaweza kuchukua muda mrefu ikiwa utaomba hii au inaweza kukusaidia. Muda mrefu zaidi wa rufaa ya haraka inaweza kuchukua ni **siku 17**.

## Je, Hukubaliani na Uamuzi wa Rufaa ya Ndani?

Unaweza kuomba Usikilizaji wa Haki katika Jimbo. Afisa anayesikiza shauri katika Bodi ya Huduma za Binadamu atasikiliza kesi yako. Wanaamua kama DVHA ilifanya uamuzi sahihi.

Mara nyingi, rufaa ya ndani lazima iwe juu ya kwanza. Kisha unaweza kuomba Usikilizaji wa Haki katika Jimbo. Je, itakuwaje ikiwa DVHA haiamui rufaa yako ya ndani kabla ya tarehe yake ya mwisho kupita? Basi unaweza kuomba masikizo ya Haki ya Jimbo bila kusubiri uamuzi.

Una **siku 120** za kuomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo. Je, siku 120 zinaanza lini? Ikiwa imeandikwa tarehe, barua hiyo inakwambia uamuzi wa rufaa ya ndani.

**Kuna njia 3 za kuomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo:**

1. **Piga simu** Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** Au piga simu kwenye Bodi ya Huduma za Binadamu moja kwa moja kwa **802-828-2536**
2. **au tuma barua** kwa:

   Bodi ya Huduma za Binadamu
   6 Baldwin St., Suite 305
   Montpelier, VT 05633-4301

**AU Mtandaoni**

**Je, tumepunguza au sitisha mafao yaduka la dawa ambazo tayari unapata?** Unaweza kuendelea na mafao yako wakati wa Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo. Lazima uombe **Ndani ya siku 11**. Siku 11 zinaanza siku DVHA ilikutumia uamuzi wake wa rufaa. Ili kuendelea kupata mafao yako, piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

**Nini kitatokea unapoomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo?** Utapata barua kutoka Bodi ya Huduma za Binadamu. Afisa anayesikiza shauri ni mtu ambaye ataamua kesi yako. Wataweka mkutano wa kusikiliza upande wako. Wataamua kama DVHA walifanya makosa. Unapaswa kushiriki katika mkutano huu. Unaweza kujisemea mwenyewe au kuwa na mwakilishi. Daktari/mtoa huduma wako anaweza kuzungumza au kutoa taarifa kwa afisa wa usikilizaji wa shauri hilo.

**Je, Unahitaji Msaada?** Unaweza kupata msaada **bila malipo** kutoka kwenye Msaada wa Kisheria wa Vermont. Piga simu kwenye Ofisi ya Utetezi wa Huduma za Afya kwa **1-800-917-7787. AU** Nenda kwenye tovuti yao.

**Itachukua muda gani kupata uamuzi kuhusu Shauri lako la Haki katika Jimbo?** Bodi ya Huduma za Binadamu lazima iamue kesi yako **ndani ya siku 90.** Siku 90 huanza tarehe ya kwanza uliyoomba rufaa ya ndani.

**Je, unahitaji uamuzi wa haraka zaidi?** Tuambie ikiwa kusubiri kutaumiza sana afya au maisha yako. Je, unakidhi kanu ni za Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo? Basi utapata uamuzi **ndani ya siku 3 za kazi**.

## Kuendelea na Mafao ya Duka la Dawa Wakati Unakata Rufaa – Mambo mengine unayopaswa kuyajua

- Je, ulilipia mafao yako mengi zaidi wewe mwenyewe? Kama **utashinda** rufaa au usikilizwaji wa shauri, unaweza kurejeshewa malipo na duka lako la dawa. Tuulize jinsi ya kufanya hivyo.
- Je, jimbo lililipia mafao wakati wa rufaa? Kama **utapoteza**, utapaswa kulipa.
- Je, unaomba rufaa au usikilizaji wa shauri? Wakati huohuo, unaweza kuomba kuendelea na huduma hadi shauri linapoisha.
- Je, rufaa yako au shauri lako ni kuhusu huduma iliyoisha au iliyositishwa? Je, iliisha au ilikatwa kwa sababu ya mabadiliko ya sheria ya serikali kuu au jimbo? Ikiwa ndivyo, **huwezi kuendelea** na huduma wakati wa rufaa au usikilizaji wa shauri.
- Je, usikilizaji wa shauri linahusu malipo yako ya kila mwezi? Lazima ulipe kabla ya tarehe inayofaa au bima yako itaisha. Kama **unashinda** shauri hilo, utarejeshewa ikiwa ulilipa kupita kiasi.

## Malalamiko

Je, hufurahishwi na mahali au wakati unaopaswa kwenda kupata huduma? Je, unafikiri huduma zako si nzuri vya kutosha? Je, ulidhurika baada ya kutumia haki zako? Je, wewe hukushughulikiwa vyema? Je, inachukua muda mrefu kupata miadi? Unaweza kuwasilisha malalamiko yanayoitwa **Malalamiko** wakati wowote. Mtu ambaye hakuwa sehemu ya kile kilichotokea kwako ataangalia malalamiko yako. Utapata barua kuhusu kile walichokipata **ndani ya siku 90**.

**Kuna njia 2 za kuwasilisha malalamiko:**

1. **Wapigie Simu** Huduma kwa Wateja kwa 1-800-250-8427.
2. **au tuma barua** kwa:

   Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont
   Timu ya Rufaa za Huduma ya Afya
   150 Pilgrim Park – 3rd Floor
   Waterbury, VT 05671-4030

Je, itakuwaje ikiwa haufurahii uamuzi wa malalamiko? Unaweza kuomba Mapitio ya Malalamiko. Mtu tofauti ataangalia Malalamiko yako na kuhakikisha sheria zilifuatwa. Utapata barua na matokeo ya ukaguzi.

Wewe na daktari wako hamuwezi kuadhibiwa kwa kukata rufaa au kuwasilisha malalamiko. Je, unahitaji msaada wa kukata rufaa au kuwasilisha malalamiko? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Unaweza pia kuuliza mwanafamili, rafiki au mtu mwingine kusaidia. Lazima uliambia Jimbo kwamba unataka mtu huyu azungumze kwa niaba yako. Tupigie simu kama unahitaji msaada kwa hatua hizi. Unaweza pia kupiga simu kwa Ofisi ya Utetezi wa Huduma za Afya kwa **1-800-917-7787**. **AU** Nenda kwenye tovuti yao.

### Sababu za Msingi na Ombi la Ugumu

Je, una VPharm? Je, una matatizo ya kujisajili kwenye mpango mpya wa dawa au kupata bima? Upigie simu mpango wa dawa au muombe mtu apige simu kwa niaba yako. Fanya kila kitu unachoweza kutatua tatizo. Itakuaje ikiwa hii haifanyi kazi? Je, itakuumiza sana ikiwa hupati dawa zako? Basi tuma Sababu za Msingi na Ombi la Ugumu. Ili kufanya hivyo, piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Wanaweza kukusaidia kupata dawa yako hadi pale tatizo litakapotatuliwa.

## Je, Unahitaji Msaada?

### Huduma kwa Wateja

Huduma kwa Wateja kukusaidia. Wanaweza kujibu maswali kuhusu mpango wako. Wanaweza kukusaidia ikiwa una matatizo ya kupata huduma za afya. Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.**

Huduma kwa Wateja ni wazi kuanzia saa 2 asubuhi (8:00a.m.) hadi saa 10:30 jioni (4:30p.m.). Jumatatu hadi Ijumaa. Hatufanyi kazi siku za sikukuu.

### Kuripoti Mabadiliko

**Lazima** uripoti mabadiliko haya **ndani ya siku 10** za mabadiliko:

- Mabadiliko ya mapato yako au kaya
- Mabadiliko ya anwani
- Kuzaliwa au kuwaasili watoto
- Vifo
- Kupata bima nyingine ya afya

### Ofisi ya Utetezi wa Huduma za Afya

Husaidia katika matatizo kuhusu huduma ya afya au mafao yako. Wanaweza pia kukusaidia katika Malalamiko, Rufaa na Usikilizaji wa Shauri la Haki. Wapigie simu kwa **1-800-917-7787**. **AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Taarifa Zaidi

Tunafurahi kuwaambia washiriki kuhusu mipango, huduma, na watoa huduma wetu. Mbali na kitabu hiki cha mwongozo, unaweza pia kupata:

- Orodha ya watoa huduma katika eneo lako ambao ni sehemu ya mipango yetu
- Kanuni za programu
- Jinsi ya kufanya huduma zetu kuwa bora
- Taarifa zaidi kuhusu huduma tunazolipia

Pia unaweza kupata maelezo zaidi kwenye tovuti.

## Mipango Mingine

Kuna mipango na huduma nyinginezo kwa watoto, watu wazima na familia. Baadhi ya mipango itakupa usafiri kwenda kwenye huduma zake. Pata maelezo zaidi kwa kupiga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Lazima utimize kanuni nyingi zaidi ili kupata baadhi ya mipango. Je, una maswali au ungependa kujua ikiwa unatimiza kanuni hizo? Piga simu kwenye mpango unaotaka. Majina na namba zao ziko hapa chini.

#### Huduma za Mchana kwa Watu Wazima

Huduma za Mchana kwa Watu Wazima huwasaidia watu wazima na watu wazima wenye ulemavu kukaa katika nyumba zao wenyewe. Huduma za Mchana kwa Watu Wazima hufanyika katika vituo vya mchana. Ni mahali salama ambapo watu wanaweza kupata huduma za afya na kijamii. Piga simu kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-2401. AU** nenda kwenye **tovuti yao**.

#### Mpango wa Huduma za Wahudumu

Mpango huu huwasaidia watu wazima wenye ulemavu wanaohitaji msaada wa kimaumbile katika shughuli za kila siku. Unawaajiri, unawafunza, unawasimamia na kupanga wahudumu wako binafsi. Piga simu kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-2401. AU** nenda kwenye **tovuti yao**.

#### Huduma Jumuishi za Watoto (CIS)

Hii husaidia wanawake ambao ni wajawazito au wale ambao wamepata mtoto. Pia, huzisaidia familia zenye watoto kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka sita. Wanasaidia kwa:

- kazi ya kijamii na msaada wa familia;

- afya ya mama/mtoto na uuguzi;
- ukuaji wa mtoto na kuwasaidia watoto kuanzia kuzaliwa hadi miaka 3 waliodumaa;
- afya ya akili ya utotoni na familia;
- huduma ya watoto; na
- mambo mengine kama vile kula vizuri, matatizo ya kuzungumza na ya lugha

Piga simu kwenye Idara ya Maendeleo ya Watoto na Familia kwa **802-241-3110** au **1-800-649-2642. AU** nenda kwenye **tovuti yao.**

### Huduma Jumuishi za Watoto - Afua ya Mapema (CIS-EI)

Mpango huu ni kwa watoto wenye umri wa miaka 3 ambao wana ulemavu. **AU** kwa watoto ambao wako nyuma ya wengine wenye umri sawa na wao. Huwasaidia watoto, watoto wachanga na familia. Piga simu kwenye Mtandao wa Familia wa Vermont kwa **1-800-800-4005**.

### Huduma za Matunzo Binafsi ya Watoto

Huduma Binafsi ya Watoto ni huduma ya Medicaid kwa watu wenye umri chini ya miaka 21. Lazima wawe na ulemavu mkubwa wa muda mrefu au tatizo la kiafya. Ni lazima iwe inawazuia kufanya mambo ambayo watu wa umri wao wanapaswa kufanya. Ni lazima wahakikishe anafanya shughuli za maisha ya kila siku, kama kula, kuvaa, kwenda bafuni pekeyake. Mpango huo husaidia kwa kutoa huduma binafsi ya mtoto. Piga simu **1-800-660-4427** au **802-863-7338. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Kliniki za Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Afya (CSHN)

Mpango huu una kliniki na husaidia kupanga huduma za watoto wenye mahitaji maalum ya afya. Wanasaidia kwa gharama za huduma za afya ambazo hazijajumuishwa kwenye bima ya afya au ya Dk. Dynasaur. Piga simu **1-800-660-4427** au **802-863-7338, AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Machaguo ya Uangalizi

Huu ni mpango wa huduma ya muda mrefu. Inalipia matunzo na msaada kwa watu wazima wa Vermont na watu wenye ulemavu wa kimaumbile. Mpango huwasaidia watu katika shughuli za kila siku. Wanaweza kuwa wanaishi nyumbani, katika matunzo yaliyoimarishwa kwenye makazi, au katika makao ya wazee. Watoa huduma ni:

- Vituo vya Mchana kwa Watu Wazima
- Mashirika ya Eneo kuhusu Wazee
- Nyumba za Kuishi Zinazosaidiwa
- Mashirika ya Afya ya Nyumbani
- Vituo vya Uuguzi
- Nyumba za Huduma za Makazi

Piga simu **802-241-0294**. **AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Huduma za Ulemavu wa Ukuaji

Huwasaidia watu wa umri wowote wenye ulemavu wa ukuaji. Huwasaidia kuishi nyumbani na familia zao. Huduma zinajumuisha usimamizi wa tatizo, huduma za ajira,

misaada ya jamii, na mapumziko. Kupumzika hutoa huduma wakati familia zinachukua mapumziko mafupi. Piga simu kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0304. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Mpango wa Msaada wa Kifedha

Huzisaidia familia kulipa gharama za huduma ya afya ya mtoto wao ambayo bima hailipii. Huduma lazima ziwe zimeagizwa au zimeidhinishwa na kliniki ya Mahitaji Maalum ya Afya ya Watoto. Piga simu kwenye Idara ya Afya ya Vermont kwa **1-800-660-4427** au **802-863-7338**. **AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Ufadhili Rahisi wa Familia

Hii ni kwa watu wa umri wowote wenye ulemavu wa ukuaji ambao wanaishi na familia. **AU** kwa familia ambazo zinaishi na kumsaidia mwanafamilia mwenye ulemavu wa ukuaji. Familia huamua ni huduma gani ambazo fedha zitalipia. Piga simu kwa Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea, Idara ya Huduma za Ukuaji kwa **802-241-0304. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Huduma za Uuguzi za Teknolojia ya Hali ya Juu

Huu ni mpango mkubwa wa uuguzi wa nyumbani. Ni kwa watu wanaohitaji teknolojia ili kuishi au wana mahitaji magumu ya kimatibabu. Mpango huu huwasaidia watu kuondoka hospitalini au kwenye taasisi hadi nyumbani kwao. Kwa watu wenye **umri zaidi ya miaka 21**, Piga simu kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0294. AU** nenda kwenye tovuti yao.

Kwa watu wenye **umri chini ya miaka 21**, piga simu kwenye Mpango wa Huduma ya Nyumbani ya Teknolojia ya Hali ya Juu ya Watoto. Piga simu **1-800-660-4427** au **802-863-7338. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Huduma za Wahudumu wa Nyumbani

Hii huwasaidia watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi wenye ulemavu. Lazima wahitaji msaada katika mahitaji binafsi au kazi za nyumbani ili kuishi nyumbani. Huduma hujumuisha ununuzi, usafi, na kufua. Wapigie simu Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0294. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Kliniki Maalum

Hizi ni kliniki za watoto. Wamebobea kwenye:

- Ugonjwa wa moyo
- Ukuaji wa Mtoto
- Craniofacial/Cleft Lip na Palate
- Fibrosisi ya Kisisti
- Ugonjwa wa kifafa/Nyurolojia
- Mkono
- Ugonjwa wa Baridi Yabisi wa Rheumatoid kwa Vijana
- Ya Umetaboli
- Myelomeningocele

- Dystrophy ya Misuli
- Utaalamu wa Mifupa
- Rhizotomia
- Magonjwa mengine

Piga simu Idara ya Afya ya Vermont kwa **1-800-464-4343** au **802-863-7200. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Huduma Maalum

Hawa ni wauguzi au wafanyakazi wa kijamii. Wanasaidia kupata huduma maalum za afya ambazo huwezi kuzipata kwenye kliniki za huduma za moja kwa moja. Piga simu Idara ya Afya ya Vermont kwa **1-800-464-4343** au **802-863-7200. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Mpango wa Vermont wa Kugundua na Afua ya Mapema wa Kusikia

Hii inatoa msaada, mafunzo na msaada wa matunzo kwa familia na watoto wao wachanga, na watoa huduma wa jamii. Wanasaidia kutafuta huduma za upimaji na afua ya mapema. Piga simu **1-800-537-0076** au **802-651-1872. AU** nenda kwenye tovuti yao.

### Afya ya Akili

Jimbo la Vermont hufanya kazi na mashirika katika jimbo zima. Husaidia watu na familia zao katika matatizo ambayo yanaharibu maisha yao. Hii inaweza kuwa tatizo kubwa la hisia, ugonjwa wa akili, au shida kubwa za tabia. Wanaweza pia kusaidia kupata huduma ya ukuaji, vitanda vya dharura, na huduma za hospitali. Piga simu Idara ya Afya ya Akili kwa **802-241-0090. AU** nenda kwenye tovuti yao. Huduma zinajumuisha:

- **Huduma za Wagonjwa wa Nje Watu Wazima** - Huduma zinaweza kujumuisha tathmini, ushauri nasaha, kuandikiwa dawa na ufuatiliaji. Inaweza kujumuisha huduma kwa watu wenye umri wa miaka 60 au zaidi wenye mahitaji ya afya ya akili. Unaweza kuwekwa kwenye orodha ya wanaosubiri.

- **Huduma za Watoto, Vijana na Familia** - Hizi ni huduma na misaada kwa familia ambazo watoto au vijana wana matatizo ya afya ya akili. Wanawasaidia kuishi, kujifunza, na kukua wakiwa na afya njema shuleni mwao na katika jamii. Huduma zinajumuisha uchunguzi, kinga, misaada ya kijamii, matibabu, ushauri na majibu ya dharura.
- **Urekebishaji na Matibabu ya Jamii** - Mpango huu huwasaidia watu kuishi katika jamii zao kwa familia, marafiki, na majirani. Huduma ni kwa watu wazima pekee wenye aina fulani za ugonjwa mkali wa akili. Lazima pia watimize kanuni zingine.
- **Huduma za Dharura -** Hizi ni huduma za dharura za afya ya akili. Ziko wazi saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Huduma zinaweza kujumuisha msaada kwa njia ya simu, ukaguzi wa ana kwa ana, rufaa, na mashauriano.

## Msaada Unapatikana 24/7

Kuanzia Huzuni hadi Mgogoro
Piga simu 988 au tuma ujumbe VT kwenda 741741

Msaada wa Wanarika
Piga simu/Tuma ujumbe kwenda 833-888-2557

Rasilimali zaidi kwenye Mentalhealth.vermont.gov VERMONT

VERMONT

Mpango wa Majeraha ya Kiwewe cha Ubongo
Mpango huu huwasaidia watu wenye umri wa miaka 16 au zaidi wenye jeraha la wastani hadi kubwa la ubongo. Unasaidia watu kurudi nyumbani kutoka hospitali na katika vituo. Huwasaidia watu kujitegemea kadri iwezekanavyo na kurudi kazini. Wapigie simu Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0294. AU** nenda kwenye tovuti yao.

**Mpango wa Wanawake, Watoto Wachanga na Watoto au WIC**
Huu ni mpango wa watoto wachanga na watoto wenye umri wa hadi miaka 5. Pia, ni kwa ajili ya watu ambao ni wajawazito au wale ambao wamepata mtoto hivi karibuni. Huwapa chakula kizuri na kuwafundisha kuhusu kula chakula bora na kunyonyesha. Mtu yeyote katika Medicaid anaweza kupata programu ya WIC. Nenda kwenye tovuti yao. **AU** tuma neno VTWIC kwenda **855-11**.

**Pata maelezo zaidi kuhusu msaada katika jamii yako nenda kwenye tovuti ya Vermont 211.**

### Je, Kuna Mtu Anaiba au Anadanganya ili Kupata Pesa za Medicaid?

Kiambie Kitengo Maalum cha Uchunguzi. Hivi ndivyo jinsi ya kuwafikia:

- **Tovuti**
  - Bofya: Ripoti Udanganyifu wa Dawa, Taka, na Dhuluma
  - Bofya: Fomu ya Rufaa ya Ulaghai na Dhuluma
- **Barua pepe:** ReportMedicaidFraud@vermont.gov
- **Simu:** 802-241-9210
- **Faksi:** 802-871-3090 (faksi ya moja kwa moja kwenda "Kitengo Maalum cha Uchunguzi cha DVHA")
- **Anwani ya Posta:**

  Kitengo Maalum cha Uchunguzi cha DVHA
  NOB 1 South, 280 State Drive
  Waterbury, VT 05671-1010